**102/2**
**Muongozo wa kusahihisha**

**UFAHAMU**

(a) – Vichafuzi ni vitu vinavyotupwa hapa na pale katika mazingira k.v mafuta kwenye fukwe za bahari, takataka na bidhaa nyinginezo.
- Ni vitu vinavyochafua mazingira. (1x 1= 1)

(b) –Viwada vinatoa mawingu makubwa ya moshi wenye sumu.
-Viwanda vimechangia kusambaa kwauchafuzi wa ardhi angani na majini (2 x 1 =2)

(c) –uchafuzi huathiri tabaka la ozoni kwa kuharibu ukanda huo kutokana na kemikal zinazotumiwa katika friji au jokofu (1 x2=2)

(d) –Mvua ya asidi huenda ikanyesha na kusababisha vifo vya mimea, kuathiri majengo na hata kuua wanyama wa porini.
- Moshi wa magari huweza kuathiri mazingira na mfumo wa akili wa binadamu.
- Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto.
- Ukanda wa ozoni ukiharibiwa miale ya jua huenda ikasababisha saratani ya ngozi inapofikia binadamu.
- Ardhi namaji yakichafuliwa huweza kuchangia vifo vya wanyama na binadamu kutokana na magonjwa mbalimbali. (zozote 4 x1=4)

(e) –miji mikubwa huwa na idadi kubwa ya ,magari ambayo hutoa moshi wenye kuchafua hewa/ anga.
-Miji mikubwa huwa na viwanda ambavyo hutoa gesi zenye madini hatari kwa maisha ya binadamu na wanyama wa pori(2x1=2)

(f) Aina za uchafuzi ni
i) Uchafuzi wa halianga – hewa / anga/ozoni
ii) Uchafuzi wa kiajali – uchafuzi unaotokea kama ajali

(g) (i) Msambao – hali ya kuenea kwa kitu/kusambaa
(ii) mazingira – eneo/ mahali tunaishi/ makazi

**UFUPISHO**

(a) Majeruhi katika ajali hufa au huathirikav vibaya au zaidi kwa sababu ya hali mbaya ya uokoaji,
- Wanaojitolea kusaidia majeruhi baada ya ajali hawatambui jinsi ya kukabiliana na uokoaji.

- Elimu inafaa kutolewa kwa kila Mkenya kurekebisha hali ya uokoaji.
- Majeruhi hubebwa hobelahobela na waokoaji bila kuzingatia madhara.
- Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha na hata kusababisha kifo.

***(zozote 5 x1 = 5 Utiririko 1=1)***

(b) –Hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji.
- Kutafuta idadi yamajeruhi
- Kuchunguza hali ya majeruhi-amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua.
- Kuchunguza jinsi majeruhi ameumia – kama kuna vidonda, kuvunjika mifupa.
- Upulizaji wa hewa kahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.
- Kumhamisha majeruhi toka eneo la ajali hadi hospitalini.
- Anza na majeruhi wenye matatizo ya kupumua iwapo majeruhi ni wengi wakati wa kuwapeleka hospitalini. (Zozote 7 x1 = 7 mtiririko 2=2=9)

3. Matumizi ya lugha

a) (i) /th/ (1 x2=2)

(ii) /o/

b) (i) Mwalimu **a**futwa kazi (Matumizi ya ‘a’)

(ii) Mwenye kitabu amefika (-enye)

(iii) Watu **hawa** wamefaulu.

(iv) **Wa** tano amefika (1 x 4=4)

c) (i) Changamano

(ii) Changamano (1 x2

(d) Kumbi zilipambwa zikapambika (al 1)

(e) (i) Ritifaa –Ng’ombe amenunuliwa (kuandika king’ong’o ng’)

- N’ nakupenda (kukata silabi katika shairi)
- ’14- ’18 (Kuonyesha tarakimu imeachua)

(1 x 1= 1)

(ii) Kistari kifupi – A-na- pig-a (kutenganisha viambishi / silabi)
- Amenunua ndizi aina ya vikomo – na –tembo (majina yanayoandikwa kwa vitengo)
- Sala-a-a-le – (kudumisha sauti)

(1 x1 = 1)

(f) Tutaona**na** – kauli ya kutendana

**na**o – kufupisha nafsi

Tu**na**posubiri – wakati ulipo

**na** – kiunganishi

**na** upishi – kihusishi (kuonyesha utendaji)

(½ x 5 = 2 ½ )

(g) Omari – yambora tendewa (sh. Kitondo)

Karo – yambwa tendwa (sh kipozi)

Hundi – yambua ala (sh. Ala)

(1 x 3 = 3)

(h) Njeri <u>**aliwalilia**</u>$^{1/2}$ marafiki <u>zake</u>$^{1/2}$ kuwa majambazi <u>**walikuwa**</u>$^{1/2}$ <u>**wamempiga**</u> ½ na kupora pesa <u>**zake**</u> ½ zote na hali <u>**yake**</u> ½ <u>**wakati huo**</u>$^{1/2}$ <u>**ilikuwa**</u> ½ mbaya.

(½ x 8=4)

(i) Mwalimu wao mgeni aliwaletea vitabu ambavyo viliwafaidi mno

S

KN KT

N V V T N S

Mwalimu Wao Mgeni aliwaletea Vitabu ambavyo viliwafaidi mno.

(al 3)

(j) (i) – pa (fanyika) - -peka (atunge sentensi )
(ii)-wa (fanyia) - -wia (sentensi)

(2 x2= 4)

(k) (i) maskinika, maskinisha n.k (sentensi)
(ii)hofia, Hofiwa n.k (sentensi) (1 x3=3)
(iii)Dhulumu (Sentensi)

(l) (i) <u>kwa kuwa alijitahidi kazini</u> <u>alifaulu</u>
KN KT
(ii) <u>Aliyenletea kitabu</u> <u>ni Yule</u>
KN KT
(iii) <u>Mwanafunzi</u> <u>aliutupa mpira uliokuwa mbaya</u>
KN KT

( ½ X 6 =3)

(m)(i) Amri (umoja) - i
(ii) Kinyonga (wingi) - wa
(iii) Ugonjwa (wingi) - ya ( ½ x 3- 1 ½ )

(n) Yeyote – kiwakilishi cha pekee
Katika – kihusishi
Wa – kivumishi cha a-ungamfu
Vizuri – kielezi (jinsi)

(o) (i) Kuliko – kulinganisha
(ii) karibu na – mahali

( 1 x2=2)

(p) Mimi sinywi chai ya mkandaa
Au
Sinyui chai ya mkandaa. (al 1)

4. Isimu Jamii

(a) (i) Krioli – Pijini iliyokomaa na kupata wazungumzaji asilia.

(ii) Pijini – Lugha iliyorahisishwa na hutumiwa na watu walio na lugha zao tofauti, \

(iii) Lingua franka – Lugha unganishi inayotumiwa na watu walio na lugha zao tofauti.

(iv) Misimu – Semi za muda na za kimaeneo

(v) Lahaja – Vilugha ndani ya lugha kuu.

( 1 x 5=5)

(b) Sifa za sajili katika muktadha wa utaalamu

- lugha hutegemea taaluma yenyewe
- huzingatia kanuni za kisarufi pamoja na uteuzi wa matumizi ya msamiati kwa dhati.
- Lugha kavu kwani hukwepa matumizi ya tamathali.
- Huonyesha adabu na heshima kwa kutajataja vyeo vya wahusika.
- Husheheni matumizi ya istilahi zinazohusiana na taaluma husika.
- Hutumia tarakimu kwa wingi.
- Hufuata utaratibu maalum unaolenga kudhihirisha ukweli au uongo wake (mantiki)
- Huchanganya ndimi wakati dhana Fulani inatiliwa mkazo.

(1x5=5)